

TAHADHARI

KAMA UNA MASHAKA KUHUSIANA NA YALIYOMO KATIKA WARAKA HUU, UNAPASWA KUMUONA DALALI WAKO WA SOKO LA HISA, MENEJA WA BENKI, MWANASHERIA, MHASIBU AU MSHAURI MWINGINE WA MAMBO YA UWEKEZAJI.

**THAMANI HALISI YA VIPANDE VYA MFUKO WA JIKIMU,
INAWeza KUONGEZEKA AU KUPUNGUA.**

MAMBO MUHIMU KUHUSU MFUKO WA KUJIKIMU

- **Madhumuni:** Mfuko huu ni mpango ulio wazi wenye lengo la kukuza na kutoa gawio kutokana na mapato ya ziada katika vipindi tofauti na pia kukuza mtaji kwa mwekezaji wa muda mrefu.
- **Chaguo la Mpango wa Uwekezaji :** Mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji - (a) Mapato ya robo mwaka (b) Mapato ya mwaka yaliyoambatanishwa na ukuaji wa vipande (growth option)
- **Nani anaruhusiwa kuwekeza:** Mfuko uko wazi kwa wataanzania walio ndani na nje ya nchi, watu binafsi, makampuni/taasisi, mabenki, asasi za kiraia (NGO) n.k. kama inavyoonyeshwa kwenye waraka huu.
- **Thamani ya Mwanzo ya Kipande:** Thamani ya mwanzo ya kipande (face value) ni Sh. 100.
- **Bei ya Kipande (Issue Price):** Vipande vitauzwa kwa bei ya Sh. 100 kwa kila kipande wakati ya mauzo ya awali (kuanzia 3 Novemba 2008 hadi 29 Novemba, 2008) na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani halisi.
- **Mipango ya mgao wa Mapato:** Mpango wa mapato kila robo mwaka na mpango wa mara moja kwa mwaka wenye gawio na ukuaji.
- **Kiwango cha Chini cha Kuwekeza:** Ni Sh. milioni 2 kwa mpango wa mapato ya robo mwaka, na Sh. milioni moja kwa mpango wa gawio kwa mwaka na Sh. 5,000 kwa mpango wa ukuaji wa mtaji kwa mwaka.
- **Uwekezaji wa Nyongeza:** Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza/unaofuata (additional investment) ni Sh.15,000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh. 5,000 kwa mpango wa ukuaji wa mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza
- **Ukwasi:** Ununuzi na Uuzaji wa vipande utafanyika kila siku ya kazi kuanzia tarehe 16 Aprili, 2009 yaani miezi minne na nusu baada ya kufungwa kwa kipindi cha mauzo ya awali. Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itatuma malipo ya mauzo ya vipande ndani ya siku 10 za kazi tangu kuwasilishwa kwa maombi ya mauzo.
- **Uwazi:** Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itafanya tathmini na kutangaza thamani halisi ya kwanza ya mfuko (Net Asset Value) katika kipindi kisichozidi siku 60 tangu kufungwa kwa mauzo ya awali na baadaye itatathmini na kutangaza kila siku ya kazi. Hali kadhalika,

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itatoa mgawanyo wa uwekezaji (Investment portfolio) kwa kila robo mwaka.

- **Uhamishaji wa Vipande:** Uhamishaji wa vipande kutoka kwenye mfuko mmoja kwenda mwingine kati ya mifuko inayoendeshwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania unaruhusiwa. Uhamishaji huu utatumia thamani halisi ya kipande kwa wakati huo bila gharama yoyote. Uhamishaji huo utafanywa kwa mauzo ya vipande kutoka kwenye mfuko mmoja na kuviwekeza kwa kununua vipande kwenye mfuko mwingine, ilimradi sifa za kuwekeza kwenye mfuko mwingine zimezingatiwa.
- **Makato ya Kodi:** Kulingana na sheria za sasa, kodi ya mapato haitotozwa kwenye gawio litokanalo na uwekezaji kwenye mfuko huu.
- **Kuorodheshwa:** Kwa sababu ni mfuko uliowazi ambapo manunuzi na mauzo ya vipande yatafanywa wakati wote na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT), vipande vya mfuko havitapendekezwa kuorodheshwa kwenye soko lolote la hisa. Hata hivyo, hapo baadaye Meneja wa mfuko, baada ya kushauriana na Mwangalizi wa Mfuko na maombi yake kupitishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, ana uwezo wa kuamua kuorodhesha vipande vya mfuko kwenye masoko ya hisa.

MFUKO WA KUJIKIMU (JIKIMU FUND)

Meneja na Mwanzilishi wa Mfuko

DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA

Jengo la Sukari, ghorofa ya pili,
Makutano ya Mtaa wa Sokoine na Ohio,
SLP 14825, DAR ES SALAAM
Tel: +255 22 2128460/2128461
Simu za Bure: (Tigo kwa Tigo) 0715 800 455 au 0715 800 544
(Voda kwa Voda) 0754 800 455 au 0754 800 544
Fax: +255 22 2137593, Email: uwekezaji@utt-tz.org
www.utt-tz.org

WATOA HUDUMA WA MFUKO WA KUJIKIMU

Mwangelizi

CRDB Bank Plc
Mtaa wa Azikiwe, Mkabala na Posta mpya
SLP 268
DAR ES SALAAM
Tel: +255 22 2117442-7
Fax: +255 22 2116714
Email: crdb@crdb.com

Msajili

DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA.
(Investor Services System)
S.L.P 14825
DAR ES SALAAM
www.utt-tz.org

Wakaguzi wa Mahesabu

KPMG
Ghorofa ya 11, PPF Tower
S.L.P 1160
DAR ES SALAAM
www.eastafrica.kpmg.com

Wanasheria

Abenry & Company
NIC Life House, S.L. P 3167
Makutano ya Mtaa wa Sokoine na Ohio,
DAR ES SALAAM
www.abenry.com

Wadhamini wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania, ambao majina yao yameorodheshwa hapa chini wanakubali kuwajibika kwa taarifa zilizomo katika waraka huu kwamba ni sahihi wakati wa tarehe ya kutolewa kwa waraka.

MAJINA YA WADHAMINI

Prof. Joseph A. Kuzilwa	-	Mwenyekiti, Bodi ya wadhamini
Mh. Omar S. Mussa (MB)	-	Mdhamini
Mh. Janet Mmari (MB/EALA)	-	Mdhamini
Bw. Ramadhani Madabida	-	Mdhamini
Bw. Ramadhani Hamisi	-	Mdhamini
Dk. Hamisi S. Kibola	-	Katibu wa Bodi / Afisa Mtendaji Mkuu

Tarehe: 3 Novemba, 2008



MFUKO WA KUJIKIMU (JIKIMU FUND)

1.0 MCHAKATO WA KUENZISHA MFUKO

UTANGULIZI

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilianzishwa tarehe 19 Juni, 2003. Tangu kuanzishwa kwake, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania imeendelea kutekeleza madhumuni yake. Mojawapo ya madhumuni ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ni kuanzisha na kuendesha mifuko ya uwekezaji wa pamoja hapa nchini. Katika kufanikisha madhumuni yake, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania imeweza kupata mafanikio yafuatayo:

MIFUKO ILIYOANZISHWA NA INAYOENDESHWA NA DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania imefanikiwa kuanzisha mifuko ya uwekezaji wa pamoja hapa nchini kama ilivyoorodheshwa katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 1

Na.	Jina la Mfuko	Tarehe ya Kuanzishwa
<u>Mfuko wa Kwanza</u>	<u>Mfuko wa Umoja</u>	<u>16 Mei, 2005</u>
<u>Mfuko wa Pili</u>	<u>Mfuko wa Wekeza Maisha</u>	<u>16 Mei, 2007</u>

Mfuko wa Umoja – Maelezo Kwa Ufupi

Ni mfuko wa kwanza wa uwekezaji wa pamoja kuanzishwa nchini, uliopata mauzo ya mwanzo makubwa katika Afrika Mashariki kwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 90.5 kutoka kwa wawekezaji zaidi ya 102,000 katika kipindi hicho.


Kupitia mfuko huu, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania imefanikiwa kumilikisha hisa kwa wataanzania wengi.

Mfuko umeweza kukidhi kwa ufanisi mkubwa mahitaji mengi ya wawekezaji waliouza vipande vyao baada ya kipindi cha kizuizi kuisha (kuanzia tarehe 1 Agosti 2006).

Hadi kufikia tarehe 20 Juni, 2008 ukubwa wa mfuko ni shilingi bilioni 64.97 ambayo ni ishara nzuri ya imani walionayo wawekezaji kwenye mfuko huu.

Mfuko umeweza kutoa gawio la shilingi 9 kwa kila kipande mwezi Septemba 2006 na baadaye, kwa utashi wa wawekezaji kubadilishwa kuwa mfuko unaokuwa (Growth Fund).

Grafu hapa chini inaonyesha faida ya mwaka wa fedha unaoanzia tarehe 2 Julai 2007 hadi tarehe 20 Juni, 2008.



Kutokana na grafu hapo juu, thamani halisi ya kipande (NAV per Unit) ilipanda kutoka shilingi 119.5424 tarehe 2 Julai 2007 hadi shilingi 140.3079 tarehe 20 Juni, 2008. Vile vile faida ya mwaka ya uwekezaji (Annualized return) inaonyesha ukuaji kutoka 7.79% kwa tarehe 3

Julai 2007 hadi 17.91% kwa tarehe 20 Juni, 2008.
Wekeza Maisha – Maelezo Kwa Ufupi

- Ni mfuko wa wazi wa uwiano wenye kuleta ukuaji wa mtaji katika kipindi cha muda mrefu ambao vilevile unatoa mafao ya Bima ya Maisha, Bima ya Ajali/Ulemavu na Gharama za Mazishi.
- Wakati wa mauzo ya awali, mfuko huu ulikusanya jumla ya Sh. 460,171,835.98 kutoka kwa wawekezaji 2,209 wenye malengo ya kujiwekea akiba (Target Amount) ya Sh. 9,764,024,000.
- Mfuko wa Wekeza Maisha ulifunguliwa tena kwa mauzo baada ya mauzo ya awali kuanzia tarehe 1 Februari 2008. Thamani halisi ya kipande cha mfuko wa Wekeza Maisha ni Sh. 110.9118 kwa tarehe 20 Juni, 2008.

1.1 MCHAKATO WA UANZISHAJI WA 'MFUKO WA KUJIKIMU'

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania(UTT) katika jitihada zake kubwa za kutoa faida ya kuridhisha kutokana na uwekezaji unaofanywa huku ikikabiliana na vikwazo mbali mbali vya hatari za uwekezaji, ina nia ya kuanzisha mifuko mbali mbali ya uwekezaji wa pamoja kwa ajili ya kukidhi matakwa ya makundi mbali mbali ya wawekezaji. Wakati wa mauzo ya mfuko wa pili wa Dhamana ujulikanao kama Wekeza Maisha, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilipata maoni toka kwa wadau mbali mbali juu ya umuhimu wa kuanzisha mfuko mwingine utakaolenga watu wanaopata vipato vya mkupuo ambao wanania ya kuwekeza ili kupata ukuaji wa mtaji (capital appreciation) na wakati huo huo kupata mapato ya mara kwa mara kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao.

Kwa wawekezaji wanaopata mapato makubwa au kwa sababu nyingine yeyote wanajikuta wamepata pato kubwa kwa mkupuo huwa

wanalazimika wao wenyewe kupanga mpango wa uwekezaji ili wapate mapato ya mara kwa mara na wakati huo huo kutaka kupata ukuaji wa mitaji yao kwa kipindi cha muda mrefu.

Ili kuweza kukidhi mahitaji ya wawekezaji wa aina hiyo, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania imeanzisha Mfuko wa Kujikimu ambao unatatua tatizo hilo la wawekezaji wa aina hiyo.

Mfuko wa Kujikimu una lengo la kutoa gawio la mapato/uwekezaji wa mapato na ukuaji wa mtaji (kama utakuwepo) kupitia uwekezaji wa muda mrefu kutokana na mseto wa uwekezaji katika hisa zilizidhoorodheshwa na dhamana zenye mapato ya kudumu.

2. UANZISHWAJI NA UENDESHAJI WA DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA

2.1 Uanzishwaji wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilianzishwa tarehe 19 Juni 2003 chini ya Sheria ya Udhhamini (Sheria ya Dhamana Na. 318).

2.2 Kazi za Wadhamini

Kazi za wadhamini miongoni mwa kazi zingine nyingi ni pamoja na:-

- Kuanzisha na kuendesha mifuko ya uwekezaji wa pamoja katika njia ambayo itaongeza thamani ya mifuko hiyo.
- Kubuni mipango mingine ya uwekezaji wa pamoja kama vile mipango ya akiba na bima au mipango mingine yoyote itakayomwezesha Mtanzania kupata mapato katika dhamana.

3. UONGOZI WA MFUKO

Mfuko wa Kujikimu utaendeshwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania. Bodi ya Wadhamini

imetayarisha muundo wa uendeshaji ili kusimamia shughuli za kila siku za mfuko huu pamoja na mifuko mingine.

3.1 Bodi ya Wadhamini

Prof. Joseph A. Kuzilwa (55)

– *Mwenyekiti, Bodi ya Wadhamini*

Bwana Joseph A. Kuzilwa ni Profesa wa Uchumi na kwa sasa ni Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe. Aliwahi kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe aliyeshughulikia Masuala ya Taaluma kuanzia Septemba 2002 hadi Septemba 2007. Vile vile amewahi kuwa Naibu Mkuu wa Chuo na Mkurugenzi wa Taaluma wa Chuo Cha Maendeleo na Utawala (IDM-Mzumbe) kuanzia mwaka 1993 hadi 1999 kabla ya chuo hicho kubadilishwa kuwa Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Profesa Kuzilwa alipata shahada yake ya kwanza ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1975. Mwaka 1978 alipata Shahada ya Uzamili ya uchumi (katika biashara za kimataifa) kutoka Chuo Kikuu cha Lancaster, Uingereza. Mwaka 1992 alipata Shahada ya Udaktari wa Falsafa katika uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Illinois, Marekani. Mwaka 2002 alipandishwa kufikia daraja la Profesa wa uchumi.

Profesa Kuzilwa ana uzoefu wa zaidi ya miaka 30 katika utawala ndani ya vyuo vikuu. Vile vile amefanya tafiti na kutoa ushauri wa aina mbali mbali katika masuala ya fedha, mipango, utawala, uchumi na biashara.

Mheshimiwa Omar S. Mussa (MB) (52)

– *Mdhamini*

Mhe. Omar S. Mussa ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Bunge la Afrika. Kabla ya kujiunga na siasa, alifanya kazi kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar- Tanzania kwa muda

wa jumla ya miaka thelathini. Alipata mafunzo yake ya Shahada ya Kwanza kutoka Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam na kufuzu Shahada ya Menejimenti na Utawala mwaka 1980. Pia mwaka 1988 alihitimu Stashahada ya Uzamili katika masuala ya fedha kutoka Chuo Kikuu cha Strathclyde huko Glasgow, Scotland.

Mwaka 1974 hadi 1984 Mh. Musa aliajiriwa kama karani wa benki na kupandishwa hadi cheo cha Meneja Utawala katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ). Baadaye aliteuliwa kuwa Kamishna wa Bajeti kuanzia mwaka 1983 mpaka 1990. Kuanzia mwaka 1991 mpaka 2000 aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ya Serikali ya Zanzibar na baadaye Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii.

Mh. Janet Mmari (MB) (56)

– *Mdhamini*

Mh. Janet Mmari ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki mwenye historia kubwa ya uhasibu. Ana Shahada ya Juu ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (CCA-1977) na (CPA-1982). Pia ana Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani na Cheti cha Juu cha uchumi kutoka Taasisi ya Uchumi ya Boulder Colorado nchini Marekani.

Mh. Mmari alijiunga na masuala ya siasa baada ya uzoefu wa miaka 20 kama Mshauri wa Mambo ya Utawala akiwa Price Water House Coopers kwa miaka 13 kama mmoja wa washauri wa ngazi za juu na baadaye kujiunga na PACE International kama mmoja wa wakurugenzi. Ni mtaalamu wa ushauri kwenye mambo yahasuyo uhasibu na ukaguzi wa mahesabu, utawala, uanzishaji na uendeshaji wa mifumo ya kompyuta.

Bwana Ramadhani Madabida (57)

– *Mdhamini*

Bwana Ramadhani Madabida amesomea sera za biashara kutoka Chuo Kikuu cha Teknolojia

cha Curtin huko Australia na kujipatia Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara mwaka 1981. Anayo Diploma ya Usimamizi wa Biashara kutoka chuo hicho cha Curtin nchini Australia.

Bwana Madabida ana uzoefu wa takribani miaka 28 katika utawala na uendeshaji wa mashirika ya umma na binafsi. Kwa hivi sasa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Tanzania Pharmaceutical Industries Limited ambayo ni mojawapo ya mashirika yaliyobinafsishwa.

Bwana Ramadhani Hamisi (52)
- Mdhamini.

Bwana Ramadhani Hamisi ni Mchumi mwenye Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1983. Pia anayo Stashahada ya Uzamili katika Maendeleo ya Uchumi kutoka katika Chuo cha United Nations Institute for Economic Development (IDEP) huko Dakar, Senegal mwaka 1994.

Mwaka 1983 aliajiriwa na Wizara ya Mipango na Uchumi kama mchumi. Mwaka 1997 aliamishwa Wizara ya Fedha akiwa Mchumi Mwandamizi.

Bwana Hamisi akiwa Hazina, alipandishwa cheo na kuwa Mchumi Mkuu kabla ya kuteuliwa kuwa Kaimu Kamishna Msaidizi wa Bajeti mwaka 2003. Tangu Novemba 2004, Bwana Hamisi amekuwa na wadhifa wa Kamishna Msaidizi wa Bajeti nafasi ambayo anayo hadi hivi sasa.

3.2 Timu Ya Utawala

DK. Hamisi S. Kibola (53)
- Afisa Mtendaji Mkuu na Katibu wa Bodi ya Wadhamini

Dk. Hamisi S. Kibola, ni Mwanasheria, mwenye Shahada ya Kwanza ya Sheria, Shahada ya Uzamili katika Sheria na Shahada

ya Udaktari wa Falsafa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ana Stashahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Amsterdam. Amefanya kazi katika sekta ya fedha nchini Tanzania kwa jumla ya miaka 16.

Bwana Alen Mchaki (55)
- Mkuu wa Utawala na Fedha

Bwana Mchaki ana Shahada ya Juu ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (CPA) na uzoefu wa zaidi ya miaka 25 iliyopatikana kutokana na mafunzo na utendaji halisi wa kazi. Kabla ya kujiunga na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania kama Mkuu wa Utawala na Fedha, alikuwa ameajiriwa na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) kama Mtaalamu Mshauri Mwandamizi, ambako alifanya kazi zaidi ya miaka 10. Mambo aliyofanikiwa kuyakamilisha akiwa PSRC ni pamoja na Ubinafsishaji wa Mashirika katika Sekta Ndogo ya Biashara, Kemikali, Saruji, Kilimo cha Mchele na Ngano, na kushiriki katika kuorodhesha Kampuni ya Bia Tanzania katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Bibi Nunu Saghaf (37)
- Mkuu wa Uendeshaji

Bibi Nunu Saghaf alijiunga na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania mwezi Februari 2005. Kama Mkuu wa Huduma kwa Wawekezaji, anasimamia vitengo mbalimbali vinavyo husiana na Huduma kwa wateja kama vile masuala ya uuzaji na ununuzi wa vipande. Bibi Saghaf alipata Stashahada ya Juu ya Uhasibu katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), alikuwa ni kiungo muhimu katika kuunda Idara ya Hazina ya ulc (Tanzania) Ltd na baadaye African Banking Corporation (ABC) Ltd kama Dalali Mwandamizi.

Bwana Rashidi K. Mchatta (38)
– *Mkuu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano*

Bwana R. Mchatta ni mtaalamu katika masuala ya Kompyuta. Alipata Shahada yake ya Sayansi (BSc) katika masuala ya Teknolojia ya Habari na Mifumo ya Utawala mwaka 1998 na Shahada ya Uzamili katika Teknolojia ya Habari na Mifumo ya Utawala mwaka 2000 kutoka Chuo Kikuu cha Zilina, Jamhuri ya Slovakia. Kabla ya kujiunga na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania Machi 2005, alifanya kazi kwenye Benki Kuu ya Tanzania.

Bwana James Washima (40)
– *Mkuu wa Uwekezaji.*

Bwana Washima ana Shahada ya Juu ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu CPA(T), Shahada ya Uzamili katika masuala ya fedha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya Kwanza ya Biashara na Uhasibu toka Chuo kikuu cha DR. B.R Ambedkar, India. Kabla ya kujiunga na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania Machi 2006, Bwana Washima alifanya kazi kwenye sekta ya tumbaku kwa miaka tisa ambako alikuwa Meneja wa Ukaguzi wa Mahesabu Kanda ya Afrika wa kampuni ya Alliance One International ambayo ni miongoni mwa makampuni yanayoongoza kwenye sekta ya tumbaku ulimwenguni.

Bwana Elikira Ndossi (62)
– *Afisa Utumishi*

Bwana Ndossi alimaliza Shahada yake ya Sanaa mwaka 1971 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Amehudhuria Kozi mbalimbali kuhusu Mashirika ya Umma, Bajeti, Utawala wa Umma na Utawala Bora.

3.3 Washauri

Inaeleweka wazi kuwa dhana ya mipango ya uwekezaji wa pamoja ni mpya hapa Tanzania;

kwa hiyo, Wadhamini wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania wamechukuwa uamuzi wa kupata msaada wa kiufundi kutoka kwa washauri wawili katika maeneo ya Uwekezaji na Uendeshaji.

Bibi Anagha Hunnurkar (49)
– *Mshauri / Uwekezaji*

Bibi Anagha Hunnurkar ana sifa katika Sheria na Uhasibu. Anayo Shahada ya Biashara (B.Com), katika Uhasibu, Stashahada ya Sheria, Stashahada ya Utawala, Stashahada ya Juu katika mambo ya Hazina na Biashara ya Fedha alizozipata katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini India. Ni mwanachama wa Taasisi ya Mambo ya Fedha ya India na pia ni Mkaguzi wa Mahesabu ya Fedha.

Bwana Jagjit Singh (42)
– *Mshauri / Uendeshaji*

Bwana Jagjit Singh ni Mtaalamu katika masuala ya Shughuli za Huduma kwa Wawekezaji. Anayo Shahada ya Uzamili katika Utawala wa Biashara (MBA) kutoka Chuo Kikuu cha Pune. Alijiunga na Dhamana ya Uwekezaji ya India kama Msaidizi wa Makamu wa Rais wa Huduma kwa Wawekezaji (Uendeshaji).

4. MWANGALIZI WA MFUKO

4.1 Muundo wa Mwangalizi

Mwangalizi wa Mfuko ni CRDB Bank Ltd ambayo ni Benki ya Biashara iliyoruhusiwa kuendesha biashara chini ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991. CRDB Bank Ltd, ni moja ya benki zinazokua kwa haraka nchini Tanzania. Ofisi yake iliyoandikishwa nchini ipo katika mtaa wa Azikiwe, S.L.P 268, Dar es Salaam.

4.2 Bodi Ya Wakurugenzi wa CRDB Bank Plc.

Bodi ya Wakurugenzi ya CRDB Bank Plc inaundwa na watu wafuatao:

Bw. Martin J. Mmari

- *Mwenyekiti, Bodi ya Wakurugenzi (Mtanzania)*

Dk. Charles S. Kimei

- *Afisa Mtendaji Mkuu (Mtanzania)*

Bw. Kai Kristoffersen

- *Mkurugenzi (Mdenishi)*

Bi. Lydia M. Joachim

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Bw. Bede P. Lyimo

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Dk. Silvia S. Temu

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Bi. Joyce N. Nyanza

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Bi. Joyce W. Luhanga

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Bi. Stergomena L. Tax

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Bw. Boniface C. Muhegi

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

Bw. Joseph C.N. Machange

- *Mkurugenzi (Mtanzania)*

4.3 Kazi za Mwangalizi

Kazi za Mwangalizi zimeelezwa katika Sheria na pia katika Waraka wa Makubaliano wa Mfuko. Kazi hizo ni pamoja na:-

a) Kusimamia na kuhakikisha usalama wa

mali za mfuko kwa niaba ya wawekezaji kulingana na vipengele vya Waraka wa Makubaliano na kuhakikisha fedha na mali zimesajiliwa kwa jina la mfuko au kwa maelekezo ya mfuko.

b) Kuwajibika kwa makosa yoyote yaliyofanywa na wakala yoyote ambaye amekabidhiwa mali ya mfuko kama vile ni makosa ya mtu aliyeteuliwa nae kuhusiana na uwekezaji uliofanywa.

c) Kuchukua hatua zinazotakiwa kuhakikisha kuwa mauzo ya mwanzo, mauzo ya baadaye, ununuzi wa vipande kutoka kwa wawekezaji na kufutwa kwa vipande kunakofanywa na mfuko vinafanywa kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano.

d) Kuhakikisha kwa uangalifu kwamba njia zitumiwazo na meneja kupata thamani ya vipande ni za kufaa, kuhakikisha bei za mauzo na manunuzi zinapatikana kwa mujibu wa Waraka wa Makubaliano.

e) Kutekeleza maagizo ya meneja kuhusiana na uwekezaji kama hayatapingana na masharti ya Waraka wa Makubaliano.

f) Kuhakikisha kwa uangalifu kuwa viwango vya uwekezaji na kukopa vya mfuko vilivyowekwa na waraka huu na matakwa yaliyoainishwa katika Sheria na taratibu zingine zinazohusu uendeshaji wa mfuko huu zinafuatwa.

g) Kwa maoni yake kutoa taarifa kwa wawekezaji itakayojumuishwa katika taarifa ya mwaka ya mfuko, kama meneja amesimamia mfuko kutokana na Waraka wa Makubaliano na kama kuna kasoro kubwa kuzitaja na kueleza hatua alizochukua.

h) Kuchukua hatua muhimu kuhakikisha kuwa hati miliki hazitolewi mpaka malipo

kamili yamefanyika.

- i) Kuhakikisha kuwa hati mbalimbali za uwekezaji zimesajiliwa kwa jina la mfuko au mteule wake kama inavyostahili.
- j) Pale ambapo miliki imehifadhiwa katika mfumo wa kompyuta, basi mwangalizi atahakikisha rasilimali hizo zinawekewa utaratibu wa kumbukumbu tofauti na mali za meneja.

5. TAMKO KUHUSU KUZINGATIA SHERIA

Inathibitishwa kwamba:

- Waraka wa Toleo hili uliotumwa kwa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ni kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania.
- Mahitaji yote ya kisheria, taratibu na maagizo yaliyotolewa na Serikali na mamlaka zinginezo katika kuanzisha Mfuko wa Kujikimu zimezingatiwa.
- Maelezo yaliyotolewa ndani ya waraka huu ni ya kweli na ya kutosha kumwezesha mwekezaji kufanya uamuzi wa busara kuwekeza katika mfuko huu.

Tarehe: 3 Novemba, 2008

Dk. Hamisi S. Kibola

Mahali: Dar es Salaam

Afisa Mtendaji Mkuu

Imetiwa sahihi na Afisa Mtendaji Mkuu

6. TAREHE MUHIMU

6.1 Ratiba ya mauzo ya mwanzo ya vipande vya MFUKO WA KUJIKIMU:

- Mwanzo wa Mauzo
- 3 Novemba, 2008 (Jumatatu)
- Mwisho wa mauzo ya mwanzo
- 29 Novemba, 2008 (Jumamosi)
- Mgawanyo wa vipande
- 30 Januari, 2009 (Ijumaa)
- Kutumwa kwa Taarifa za umiliki wa vipande kwa wawekezaji
- 10 Februari, 2009 (Jumanne)

Kwa namna yeyote ile kipindi cha mauzo ya mwanzo hakitaongezwa kwa sababu inaweza kuleta athari kwa wawekezaji kukosa imani na kuathiri maendeleo ya soko.

7. GHARAMA ZA TOLEO LA KWANZA

Gharama za kuanzisha Mfuko wa Kujikimu ni kama ifuatavyo:-

- Elimu kwa umma, Matangazo na Gharama za Masoko
- Gharama za wakala
- Gharama za uchapaji, posta na maandalizi ya taarifa za wawekezaji
- Gharama za huduma za wanasheria na wakaguzi wa mahesabu
- Gharama Nyinginezo

Gharama hizi za toleo la kwanza zitalipwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ambaye ni mdhamini na Meneja wa mfuko. Gharama zote hizi hazitalipwa na mfuko na hivyo hakutakuwa na gharama kwa mwekezaji anayeingia kwenye mfuko (No entry load).

8. HATARI ZA UWEKEZAJI

Mwekezaji anapaswa kutambua kwamba uwekezaji wa rasilimali za mfuko unakabiliwa na mashaka yanayoweza kuathiri hali ya mfuko siku hadi siku hivyo kuweza kusababisha kupanda au kushuka kwa

thamani halisi ya mfuko kutegemea uwekezaji.

Wawekezaji sharti watambue, miongoni mwa mambo mengine kwamba:

- Ufanisi wa makampuni ambayo mfuko umewekeza katika hisa zake za kawaida unaweza kudorora au kuendelea.
- Mbali na dhamana za serikali, dhamana zingine zilizotolewa na makampuni ya sekta binafsi, zinaweza kushindwa kulipa deni.
- Mabadiliko ya viwango vya riba vinaweza kuathiri thamani ya dhamana zenye mapato yasiyobadilika ambazo zime wekezwa na mfuko.
- Mabadiliko katika viwango vya kubadili fedha yanaweza kuathiri thamani ya rasilimali za mfuko katika dhamana zilizo katika fedha za kigeni (hapo Serikali itakaporuhusu mfuko kuwekeza nje ya nchi).
- Hali ya ukwasi katika Soko la Hisa la Dar Es Salaam inaweza kusababisha kushuka kwa thamani ya mfuko.
- Utaratibu wa kodi zinazotowazwa katika mapato ya dhamana za uwekezaji unaweza kubadilika, hivyo kuathiri mapato ya mfuko pamoja na mapato kwa mwekezaji.
- Mazingira mengine yasiyoweza kutabirika mapema ambayo yanaweza kuathiri rasilimali zilizowekezwa na Mfuko wa Kujikimu.

9. MFUKO WENYE KUTOA GAWIO NA KUKUA KWA MTAJI (KUJIKIMU)

MFUKO WA KUJIKIMU

MAELEZO KWA UFUPI: Mfuko wa Kujikimu umeanzishwa ili kumuwezesha mwekezaji kupata uwekezaji wenye mpangilio. Katika mazingira ambayo kuna nafasi kubwa ya kuboresha kipato baada ya kustaafu, ni wajibu kwa kila mmoja kupanga mwenyewe maisha ya uzeeni. Kwa kutumia nguvu ndogo katika kufanya mipango, kila mmoja ana nafasi ya kuhakikisha kwamba ataishi maisha mazuri mara baada ya kustaafu.

Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) baada ya kufanya tathmini imejikita kuleta Mfuko wa Kujikimu uliofanyiwa uhakiki wa kiwango cha juu, ili kuweza kuziba pengo hili kwa wawekezaji.

Ukweli ni kwamba, ni watu wachache wenye kuelewa hali halisi ya maisha baada ya kustaafu. Ni wachache wanaoelewa ni kiasi gani waweke akiba, kiasi gani watahitaji hapo baadaye, ni namna gani mfumuko wa bei unaweza kuwaathiri au ni namna gani mtindo wa maisha yao kwa ujumla unaweza kubadilika.

Mambo yatolewayo na Mfuko: MFUKO WA KUJIKIMU ni utatuzi wa kifedha unaolenga kuwezesha utaratibu wa mtiririko wa mapato ya mara kwa mara ambayo yatawasaidia wawekezaji kuweza kukidhi mahitaji yao kwa mpangilio unaoeleweka. Vile vile una lengo la kuleta maisha mazuri ya wastaafu kwa kutoa nyongeza katika malipo yao ya wastaafu kwa kutoa mapato ya mara kwa mara (regular income) huku ukihakikisha kiasi kilichowekeza kwa mkupuo (lump sum amount) kikibakia bila kupungua.

9.1 MALENGO YA MFUKO

- Mfuko wa Kujikimu unalenga kutatua tatizo la kifedha kwa wawekezaji ambao wanahitaji mapato ya mara kwa mara na wakati huo huo wakiangalia uwezekano wa kupata ukuaji wa mitaji yao kwa muda mrefu.

- Mfuko wa Kujikimu unalenga kuhamasisha umuhimu wa kupanga utaratibu wa uwekezaji na kuleta mfuko ambao utasimamiwa na Meneja ambaye anauzoefu wa kuendesha mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

9.2 NANI ANARUHUSIWA KUWEKEZA KATIKA MFUKO

- Mtanzania aliye ndani au nje ya nchi anaweza kujiunga yeye mwenyewe (single) au kujiunga na mwenzake (jointly) au kwa mpango wa 'mmojawapo kati ya wamiliki wawili' (either or survivor basis); Maelezo: Iwapo umiliki ni wa watu wawili (Joint Holding) basi wote wawili watapaswa kuweka sahihi zao wakati wa kujaza fomu kwa ajili ya maombi yeyote. Iwapo ni katika utaratibu wa 'mmojawapo kati ya wamiliki wawili' (either or survivor basis) basi yeyote kati yao anaweza kuweka sahihi yake kwa ajili ya maombi yeyote na malipo yatoanayo na mauzo ya vipande kwa Meneja yatalipwa kwa aliyeweka saini kwenye fomu. Hii imewekwa ili kuwawezesha wastaafu wasipate usumbumbu wakati wa kushughulikia uwekezaji wao.
- Watoto wa kitanzania kupitia kwa mzazi au mlezi anayetambulika kisheria.
- Watu binafsi wanaomiliki kampuni kwa pamoja (Partnership firms);
- Makampuni/Taasisi, mabenki, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Vyama vya Ushirika, makundi ya jamii yaliyosajiliwa nchini
- Mabenki na Taasisi za fedha, Taasisi za Kidini na vyama vya hiari, Wakfu au Dhamana za Binafsi (kwa maombi yao kupitishwa/ kupokelewa), Dhamana za Binafsi iwapo zinaruhusiwa kuwekeza kwenye mifuko ya dhamana kutokana na

mikataba yao ya makubaliano (trust deeds)

- Makampuni, Taasisi na makundi mengineyo kama ambavyo itakavyoamuliwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) ilimradi itafuata sheria za Masoko ya Mitaji na Dhamana;

9.3 MUDA WA UWEKEZAJI

- Mfuko ni wa wazi na mwekezaji anaweza kuwekeza kwa muda wowote atakaopenda;

9.4 KIWANGO CHA CHINI CHA KUWEKEZA

- Kiwango cha chini cha kuwekeza ni kama ifuatavyo –
 - Sh. 1,000,000/- kwa wale waliopo katika 'Mpango wa Gawio(Mapato) kwa mwaka' (Annual Income plan)
 - Sh. 2,000,000/- Kwa wale waliopo katika 'Mpango wa Gawio(Mapato) kwa kila robo mwaka' (Quarterly Income plan)
 - Sh. 5,000/- Kwa wale waliopo katika 'Mpango wa mwaka wa Kukua' (Annual Reinvestment plan)
- Hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza
- Uwekezaji wa Nyongeza (Additional Investment)
 - Kiasi cha Sh. 15,000/- kwa mwekezaji aliye katika mpango wa gawio (mapato);pasipo ukomo.
 - Kiasi cha Sh. 5,000/- kwa mwekezaji aliye katika mpango wa mwaka wa kukua;pasipo ukomo.

Hakuna ukomo wa lengo la ukubwa wa Mfuko huu, hivyo basi iwapo maombi yote yatakidhi

mahitaji ya Waraka huu, basi maombi yote yatagawiwa idadi ya vipande vitakavyoombwa kulingana na pesa yote iliyowasilishwa kwa ajili ya kuwekezwa.

9.5 AINA YA MIPANGO YA UWEKEZAJI

Mfuko una mipango mitatu ya uwekezaji kulingana na namba ya mgawanyo wa mapato (gawio) kama ifuatavyo:

- Mpango wa mgawanyo wa gawio (mapato) kwa kila robo mwaka (Quarterly Income Distribution Plan)
- Mpango wa mgawanyo wa gawio (mapato) kwa kila mwaka (Annual Income Distribution Plan)
- Mpango wa mwaka wa Kukua (Annual Reinvestment Plan)

Mfuko unatoa fursa ya Mpango wa mwaka (Annual Reinvestment Plan) wa kukua kwa ajili ya kuwawezesha wawekezaji wadogo kushiriki.

Mfuko unaweza kutoa mipango mingine ya uwekezaji huko mbeleni.

Kiasi cha pesa zote zitazokusanywa kutoka katika mipango hiyo ya uwekezaji, zitawekezwa kwa pamoja. Wawekezaji wanashauriwa kuonyesha chaguzi zao za mipango hiyo ya uwekezaji wanapojaza fomu za maombi. Iwapo fomu halali itawakilishwa bila ya mwekezaji kuonyesha ni chaguzi gani anayoipendelea, basi Meneja wa Mfuko ataiweka katika Mpango wa mwaka wa kukua.

Vile vile, wawekezaji wanashauriwa kujaza fomu zaidi ya moja iwapo watataka kuwekeza katika mipango mbali mbali ya uwekezaji wa Mfuko wa Kujikimu.

9.6 BEI YA KIPANDE (ISSUE PRICE)

- Mauzo ya awali – Vipande vitauzwa kwa bei ya Sh. 100 kwa kila kipande wakati ya mauzo ya awali (kwa vile gharama wakati wa mauzo ya mwanzo zitalipwa na Meneja wa mfuko);
- Mauzo yatayofuata – Vipande vitauzwa kulingana na thamani halisi ya kipande (hakutakuwa na gharama za kuingia kwenye mfuko).

Muhimu: Baada ya mauzo ya mwanzo, mfuko utakuwa wazi kwa mauzo kuanzia tarehe 16 Aprili, 2009.

10. GHARAMA ZA KUINGIA KWENYE MFUKO: HAZITOKUWEPO

11. GHARAMA ZA KUJITO A KWENYE MFUKO.

Mfuko unawavutia wawekezaji wa muda mrefu na unatambua umuhimu wa mfuko kuwa na ukwasi. Kwa maana hiyo, gharama za kujitoka kwenye mfuko ziko kwa viwango mbali mbali kama ifuatavyo:

- Ndani ya mwaka mmoja tangu tarehe ya kuwekeza: 2% ya thamani halisi ya kipande
- Zaidi ya mwaka wa kwanza na chini ya mwaka wa pili tangu tarehe ya kuwekeza: 1.5% ya thamani halisi ya kipande
- Zaidi ya mwaka wa pili na chini ya mwaka wa tatu tangu tarehe ya kuwekeza: 1% ya thamani halisi ya kipande
- Baada ya miaka mitatu tangu tarehe ya kuwekeza: Hakuna gharama za kutoka.

12. UKWASI-UNUNUZI WA VIPANDE.

Mfuko unatoa fursa ya kuuza vipande kuanzia tarehe 16 Aprili 2009, kwa kuzingatia taratibu

na gharama za kujitoa kama zilivyoonyeshwa ibara 11 ya waraka wa toleo na utaratibu wakati wa kipindi cha kizuizi kama ifuatavyo;

1. Mwekezaji aliyejiunga na mfuko wakati wa mauzo ya awali ataruhusiwa kuuza vipande vyake kuanzia tarehe 16 Aprili 2009.
2. Wawekezaji wote watakoingia baada ya mauzo ya awali wataweza kuwa na sifa ya kuuza kama ifuatavyo.

Tarehe za Kujiunga	Kipindi cha Kizuizi	Wakati wa kuanza Kuuza Vipande
Kuanzia tarehe 1, Januari mpaka tarehe 31, Machi	Mpaka tarehe 30, June	Julai
Kuanzia tarehe 1, Aprili mpaka 30, Juni	Mpaka tarehe 30, Septemba	Octoba
Kuanzia tarehe 1, Julai mpaka tarehe 30, Septemba	Mpaka tarehe 31, Desemba	Januari
Kuanzia tarehe 1, Oktoba mpaka 31, Desemba	Mpaka tarehe 31, Machi	Aprili

13. MASHARTI YA KUJIUNGA NA MFUKO WA KUJIKIMU.

Kila mwekezaji mwenye sifa na nia ya kushiriki katika Mfuko huu anatakiwa afuate yafuatayo:-

- a) Kujaza fomu ya ununuzi wa vipande kama inavyoelezwa na Meneja wa mfuko.
- b) Kulipa kiasi kinachotakiwa kwa ajili ya kujiunga kulingana na mpango aliouchagua.

14. MGAO WA VIPANDE (ALLOTMENT OF UNITS)

Hakuna ukomo wa lengo la ukubwa wa Mfuko huu, hivyo basi iwapo maombi yote yatakidhi mahitaji ya Waraka huu, basi maombi yote yatagawiwa idadi ya vipande vilivyoombwa kulingana na pesa yote iliyowasilishwa kwa ajili ya kuwekezwa.

Vipande vitatolewa kwa tarakimu nne za desimali. Mgao wa vipande utatolewa kulingana na kiasi kilichowekezwa kwa Meneja pamoja na fomu ya maombi iliyokamilika.

15. TAARIFA YA AKAUNTI.

Taarifa ya akaunti itatolewa ikiwa inaonyesha idadi ya vipande anavyomiliki mwekezaji. Meneja atatoa na kutuma taarifa za akaunti ndani ya siku kumi za kazi kwa mauzo ya vipande yatakayofanywa baada ya kipindi cha awali cha mauzo (baada ya kizuizi). Taarifa za akaunti za wawekezaji watakojiunga na mfuko kwenye mauzo ya awali zitatolewa na kutumwa kama ilivyoonyeshwa kwenye kipengele cha 6.1 cha waraka huu; yaani tarehe 10 Februari, 2009 (Jumanne).

Taarifa za akaunti za mwaka zitatolewa zikionyesha kiasi cha nyongeza kilicho wekezwa (kama kipo), vipande vilivyopungua kutokana na uuzaji, vipande vilivyoongezeka (kutegemeana na mpango) na idadi ya vipande vilivyopo.

Kwa maana nyingine, taarifa ya akaunti itakuwa ni taarifa fupi inayoonyesha taarifa zote za mwaka mzima za akaunti ya mwekezaji.

Taarifa ya Akaunti inaweza kutolewa pale ambapo mwekezaji atafanya maombi maalum. Hata hivyo, Meneja anayo haki ya kutoza kiasi kidogo cha ada cha kati ya Sh. 800 hadi 3,000 kwa ajili ya huduma hiyo. Taarifa ya akaunti zitatolewa ndani ya siku tatu mara baada ya maombi kuwasilishwa ofisi za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania

16. KUGAWANYWA KWA VIPANDE (SPLIT OF UNITS)

- a) Mgawanyiko wa vipande ni utaratibu ambapo thamani ya kipande itagawanywa;
- b) Vipande vinaweza kugawanywa miongoni mwa wawekezaji kadri itakavyoamuliwa na Meneja wa mfuko kwa kuzingatia masilahi ya wawekezaji na Mfuko, baada ya kupata ruhusa kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana;

- c) Mgawanyiko wa vipande utakapofanyika, utakuwa sawia na miliki ya vipande vya mwenye vipande vitakavyokuwepo siku ya mgawanyo;
- d) Kuhusu haki na stahili juu ya vipande vya mgawanyo, itakuwa sawa na vipande vya mwenye vipande vilivyo orodheshwa kwenye daftari la Mfuko siku ya mgawanyo;
- e) Kufuatia mgawanyo wa vipande, thamani ya kipande itashuka sawa na thamani ya vipande vilivyogawanywa. Hata hivyo, thamani ya jumla ya vipande vya mwekezaji kabla na baada ya mgawanyo haitabadilika;
- f) Taarifa ya akaunti yenye kuonyesha salio la vipande itatolewa kwa wawekezaji waliopata mgawanyo;
- g) Ni wawekezaji wale tu watakaokuwa wamesajiliwa kwenye Daftari la wenye vipande siku ya mgawanyo wa vipande watastahili kupata vipande vya mgawanyo.

17. UTEUZI WA MWAKILISHI.

- a) Uteuzi wa mwakilishi/mrithi unaruhusiwa katika mfuko huu.
- b) Pale ambapo vipande vinamilikiwa na watu wawili katika umiliki wa pamoja au katika utaratibu "mmoja wapo kati ya wamiliki wawili" wanayo haki ya kuchagua mwakilishi/mrithi wa vipande vyao ambaye atakuwa na haki ya umiliki pale ambapo wawekezaji hao wawili watakapokuwa wamefariki;
- c) Wamiliki wasio watu binafsi hawawezi kumchagua mwakilishi/mrithi;
- d) Suala la usimamizi wa vipande kwa niaba ya mtu, litakoma punde vipande vitakapouzwa;
- e) Mwakilishi/mrithi anaweza kuondolewa na wanaomiliki vipande na ambao mwanzo walimteua. Pale ambapo mwakilishi ameondolewa, meneja hana wajibu wa kuhamisha vipande kwenda kwa mwakilishi;
- f) Ni mtu mmoja tu ambaye ni raia wa Tanzania pamoja na watoto (akiwakilishwa na mzazi/mlezi) anaweza kuchaguliwa kama ilivyo kwenye fomu ya maombi;
- g) Wakati wa kumuandikisha mwakilishi/mrithi, Meneja wa Mfuko atathibitisha taarifa hiyo kupitia kwenye Taarifa ya Akaunti au kwa barua maalum kama itakavyo amuliwa na meneja;
- h) Mwakilishi/mrithi anaweza kubadilishwa na mmiliki wa vipande katika kipindi chochote wakati wa uwepo wa uwekezaji;
- i) Iwapo mmiliki wa vipande atafariki, vipande vitamilikishwa kwa mwakilishi kwa kufuata taratibu kama zilivyoanishwa, madai ya kifo yatalipwa kwa mwakilishi kulingana na vipande vilivyomilikishwa, ukizingatia gharama zote zilizotokana na vipande hivyo.
- j) Ikumbukwe kwamba uteuzi wa mwakilishi ndani ya mfuko huu utazingatia vipengele vingine vya sheria za nchi. Uwepo wa huduma hii haumaanishi Meneja wa Mfuko anajaribu kumpa mwakilishi haki nyingine za ziada zaidi ya zile zilizopo kisheria.
- k) Uwakilishi wa vipande katika mfuko hausababishi kutengeneza mazingira ya kupata mali za mwenye vipande inapotokea mwenye vipande amepoteza maisha. Mwakilishi atapokea vipande kama wakala na msimamizi tu kwa ajili ya warithi halali kisheria. Inaelezewa zaidi

hapa kwamba mwakilishi chini ya huduma ya uwakilishi inayotolewa na mfuko huu sio lazima atambulike/apate faida yeyote ile kwenye vipande kutokana na uwakilishi wake wa vipande hivyo.

- l) Inapotokea migongano/ugomvi kati ya warithi inayopelekea mashitaka hadi maamuzi ya mahakama yanayoelekeza ugawanyaji wa vipande; tofauti na ule uliopo kwenye uwakilishi, basi maamuzi ya mahakama yatakuwa ndiyo ya mwisho.

18. KUHAWILISHA/KUHAMISHA VIPANDE.

Vipande vya mfuko vinaweza kuhamishika na kuhawilishwa.

19. KUWEKA REHANI /KUHAMISHA VIPANDE

- a) Uwekaji rehani au uhamishaji wa vipande unaruhusiwa pale unapohusisha benki au taasisi za fedha. Wenye vipande wanaweza kuweka rehani au kuhamisha vipande vyao kama njia ya kuombea mikopo. Mwekezaji atapaswa kujaza fomu ya maombi ya kuweka rehani vipande vyake na kufuata taratibu nyingine kama zitakavyoelekezwa.
- b) Benki au taasisi ya fedha iliyotoa mkopo ina haki ya kuuza vipande kwa Meneja au kuhamisha vipande hivyo kwa ajili ya kulipa mkopo iliutoa pindi mwenye vipande atakaposhindwa kurejesha mkopo katika muda waliokubaliana.
- c) Vipande vilivyowekwa rehani havita ruhuswa kuuzwa/kuhamishwa/ kubadilishwa mpaka viambatanishwe na uthibitisho wa kulipwa kwa mkopo.

20. KUHAMISHA VIPANDE KUTOKA MFUKO MMOJA KWENDA MWINGINE

Uhamishaji wa vipande kutoka mfuko mmoja kwenda mwingine kati ya mifuko inayoendeshwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania unaruhusiwa. Uhamishaji huu utatumia thamani halisi ya kipande kwa wakati huo bila gharama yoyote. Uhamishaji huo utafanywa kwa mauzo ya vipande kutoka kwenye mfuko mmoja na kuviwekeza kwenye mfuko mwingine kwa kununua vipande kwenye mfuko mwingine, ilimradi sifa za kuwekeza kwenye mfuko mwingine zimezingatiwa.

Muhimu:

- a) Pale mwekezaji anapohama kutoka kwenye mfuko huu (Mfuko wa Kujikimu) hatastahili kupata faida zozote zitokanazo na mfuko huo.
- b) Kuhama kutoka kwenye mfuko kabla ya kutolewa kwa taarifa za akaunti ya mwekezaji wakati wa mauzo ya mwanzo au yanayofuata hakuruhusiwi.
- c) Kuhamia kutoka kwenye mifuko mingine ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) wakati wa mauzo ya mwanzo hakuruhusiwi.

21. MGAWANYO WA MAPATO

Kulingana na uwepo wa mapato, mgawanyo wa mapato utafanywa na Meneja baada ya kushauriana na Mwangalizi wa mfuko kila robo ya mwaka/ mara moja kwa mwaka au kwa mfumo wowote ule kama itakavyokuwa hapo baadaye (kuzingatia utashi wa mwenye vipande).

Mwenye vipande ambaye jina lake litakuwepo kwenye kumbukumbu za vitabu vya mfuko katika siku iliyochaguliwa ya mgawanyo wa mapato, na ambaye yupo kwenye mpango wa mapato wa robo mwaka ndiye atakayestahili mgao wa fedha taslimu.

Wenye vipande waliopo kwenye mpango wa mapato wa mwaka hawatapata gawio lolote kwenye robo tatu za mwaka za mwanzo na badala yake mapato yao ya vipindi hivyo yatatumika kununulia vipande vya nyongeza kwenye mfuko kwa thamani halisi ya kipande. Mwisho wa robo ya nne (robo ya mwisho wa mwaka) kwa tarehe husika, vile vipande vya nyongeza vilivyopatikana kwenye robo zote nne vitanunuliwa na mfuko na mapato yake yatahesabika kama mapato ya mwaka ya mwenye vipande.

Kwenye mgawanyo wa mapato, thamani halisi ya kipande itapungua kulingana na kiasi cha mgao wa mapato.

Kwa wenye vipande watakaokuwa wamechagua mpango wa kukua (growth option). Hawatapata mgao wa mapato na badala yake mapato waliyostahili kupokea yatatumika kununulia vipande vya nyongeza kwa thamani halisi ya wakati huo.

Mwenye vipande ambaye hakuonyesha chaguo lake katika fomu ya maombi atachukuliwa kama amechagua mpango wa kukua.

Mgawanyo wa mapato kwa wenye vipande ambao taarifa zao za benki zinajulikana watalipwa kwa kutumiwa fedha kwenye akaunti zao za benki na kwa wale ambao hawajatoa taarifa zao za benki watalipwa kwa njia ya posta(hawala ya posta).

Malipo ya benki au kwa njia ya posta yatafanyika ndani ya siku kumi za kazi kutoka tarehe ya gawio. Meneja atatuma taarifa za akaunti (SOA) kwa wenye vipande waliopata vipande vya nyongeza chini ya mpango wa kukua baada ya siku kumi tangu tarehe ya gawio.

22. RATIBA YA MGAWANYO WA MAPATO.

22.1 Mpango wa mapato wa robo mwaka:

Kwenye mpango huu wa mapato, mgawanyo wa mapato utatangazwa kila tarehe ya siku ya kazi ya mwisho ya kila robo mwaka, mfano tarehe ya siku ya kazi ya mwisho kwa robo iishiyo mwezi Machi, Juni, Septemba na Desemba. Mfuko una malengo ya kutoa mapato mara kwa mara kwenye mpango wa mapato kwa robo mwaka. Hata hivyo hakuna uhakika mwekezaji atapata kiasi gani cha gawio au mgao mara kwa mara. Ratiba ya mgawanyo wa mapato ya mpango wa mapato wa robo mwaka itakuwa kama inavyo onyeshwa hapo chini:

Tarehe ya Mwekezaji Kujiunga na Mfuko (*)	Tarehe iliyopangwa ya gawio la mapato. (Siku ya kazi ya mwisho kwa mwezi)	Tarehe ya Malipo ya gawio
Januari – Machi	Machi	Ndani ya siku 10 za kazi toka tarehe iliyopangwa ya gawio la mapato.
Aprili – Juni	Juni	
Julai – Septemba	Septemba	
Octoba – Desemba	Desemba	

(*) Muhimu:

- Mwaka wa fedha wa Mfuko utanzia Julai mosi mpaka Juni 30 ya kila mwaka;
- Kwa vile Mfuko una kipindi cha utulivu cha miezi mine na nusu (kitaishia tarehe 15 Aprili 2009), kutakuwa na upendeleo maalum kwa wenye vipande watakojiunga na Mfuko wakati wa mauzo ya mwanzo, ambapo malipo ya mapato kwa mpango wa robo mwaka yatatangazwa tarehe 1 Mei, 2009 na malipo yatafanyika ndani ya siku kumi za kazi kutoka tarehe hiyo. Gawio hilo litatolewa kutokana na faida itakayopatikana kwenye mfuko hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2009.
- Hata hivyo, Mfuko utafuata tarehe hizo (hapo juu) kwa ajili ya malipo ya gawio chini ya mpango wa robo mwaka.

22.2 Chaguo la Mwaka:

Chini ya chaguo hili, tarehe ya kupewa gawio kwa mwekezaji itakuwa ni siku ya mwisho ya mwaka wa fedha wa mfuko ambayo itakuwa ni Juni 30 ya kila mwaka. Hata hivyo hakuna uhakika mwekezaji atapata kiasi gani cha gawio au mgao. Hata hivyo ifahamike kuwa ni

lengo la Mfuko kutoa gawio kila mwaka. Tarehe za kutoa gawio chini ya mpango wa gawio la kila mwaka ni kama ifuatavyo:

kipindi cha kufunga vitabu ambacho hakitazidi siku saba za kazi na bila kuzidi siku kumi na tano kwa mwaka.

Tarehe ya Mwekezaji Kujiunga na Mfuko (*)	Tarehe iliyopangwa ya gawio la mapato. (Siku ya kazi ya mwisho kwa mwezi)	Tarehe ya Malipo ya gawio
Julai 1 hadi Juni 30 ya [mwaka wowote]	Juni 30 [ya kila Mwaka]	Ndani ya siku 10 za kazi toka tarehe iliyopangwa ya mgawanyo wa mapato.
(*) Muhimu: - Mwaka wa fedha wa Mfuko utanzia Julai mosi mpaka Juni 30 ya kila mwaka; - Kwa wale wawekezaji ambao watajiunga na mfuko wakati wa mauzo ya awali, uwekezaji wao wa kwanza katika mpango wa gawio la mwaka utanzia tarehe 30 Juni 2009 na gawio hilo litalipwa ndani ya siku 10 za kazi kuanzia tarehe hiyo. Gawio hilo litatolewa kutokana na faida itakayopatikana kwenye mfuko mpaka mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2009; - Hata hivyo, Mfuko utafuata tarehe hizo (hapo juu) kwa ajili ya malipo ya gawio chini ya mpango wa Mwaka.		

Mauzo ya mwanzo yatafanyika kuanzia 3 Novemba 2008 mpaka 29 Novemba, 2008.

24.2 MAUZO YANAWEZA KUFANYIKA SEHEMU ZIFUATAZO

Maombi ya kununulia vipande wakati wa mauzo ya mwanzo yanaweza wakilishwa kwa mawakala wetu katika sehemu zifuatazo:

- Tawi lolotela CRDB Bank Plc.;
- Tawi lolote la Akiba Commercial Bank Ltd.;
- Tawi lolote la Exim Bank (Tanzania) Limited;
- Tawi lolote la Benki ya Posta;
- Ofisi yoyote ya Shirika la Posta au
- Ofisi za madalali waliosajiliwa wa Soko la Hisa la Dar es Salaam: Tanzania Securities Ltd, Solomon Securities Ltd, Rasilimali Ltd, Orbit Securities, Vertex International Securities Ltd & Core Securities Ltd,

23. UBADILISHAJI WA MPANGO

Katika Mfuko huu, mwekezaji anaruhusiwa kubadilisha uwekezaji wake kutoka kwenye mpango wa gawio na kuwa mpango wa kukua au vinginevyo katika muda na wakati utakaoamuliwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT). Mwanzoni, hili litafanyika kwa kila robo mwaka na baadaye kwa kila mwezi.

Mabadiliko haya yataruhusiwa bila gharama zozote.

Maombi ya kubadilisha mpango yatafanywa kwa kujaza Fomu ya Maombi ya Mabadiliko (Change – Over Form).

24. UNUNUZI WA VIPANDE

24.1 LINI VIPANDE VINAWEZA KUNUNULIWA

Vipande vinaweza kununuliwa siku yoyote ya kazi wakati wa mauzo ya mwanzo na baada ya kipindi cha utulivu (cool off period) isipokuwa

Maombi kwa ajili ya mauzo baada ya kipindi cha utulivu (cool off period) yanaweza kufanywa katika ofisi yoyote iliyoteuliwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT).

24.3 MALIPO KWA AJILI YA UNUNUZI WA VIPANDE

Malipo kwa ajili ya mauzo ya mwanzo ya vipande yanaweza kufanywa kwa mmojawapo wa mawakala waliotajwa hapo juu kwa fedha taslim au hundi ya benki ambayo italipwa kwenye akaunti ya mfuko “AKAUNTI YA MFUKO WA KUJIKIMU”,

Kumbuka: Hakuna malipo taslim kuhusiana na ununuzi wa vipande katika mfuko yatakayofanywa kwa chombo chochote cha kati mbali na mawakala waliotajwa hapo juu.

25. UTARATIBU WA MAUZO NA MANUNUZI YA VIPANDE BAADA YA MAUZO YA AWALI (SUBSEQUENT SALE AND REPURCHASES)

25.1 MAUZO YANAYOFUATA (SUBSEQUENT SALE OF UNITS)

Mauzo ya vipande baada ya Mauzo ya Mwanzo yataanza baada ya muda wa utulivu (cool off period) wa miezi minne na nusu, kuanzia tarehe 16 Aprili 2009. Kuanzia tarehe hii, Meneja atauza vipande kwa thamani halisi ya kipande ya wakati huo. Meneja ataendelea kuuza vipande kwa utaratibu ufuatao:

- a) Mauzo ya vipande yatafanyika kwa thamani ya kipande kwa wakati huo bila gharama yoyote ya nyongeza;
- b) Mwekezaji anatakiwa kuzingatia thamani halisi ya kipande wakati anatafakari kununua vipande vya Mfuko wa Kujikimu. Iwapo atakuwa na mashaka anashauriwa kupata ushauri kutoka kwa wataalam wa maswala ya fedha;
- c) Iwapo mwekezaji anaamua kununua vipande, atapaswa aende kwa wakala walioteuliwa na Meneja wa Mfuko na atapewa fomu ya maombi na taarifa nyinginezo;
- d) Mwekezaji atapaswa kujaza fomu ya maombi ya kununua vipande vya Mfuko wa Kujikimu;
- e) Fomu ya maombi ipelekwe kwa wakala yeyote aliyeteuliwa na Meneja wa Mfuko pamoja na viambatanisho vifuatavyo:

- Fedha taslimu (fedha za kitanzania)
- Hundi ya Benki iliyofungwa - ambayo italipwa kwa "Mfuko wa Kujikimu"

f) Maombi ya mauzo ya vipande yatachukuliwa yamepokelewa siku husika ikiwa tu yatakuwa yamepokelewa na kukubaliwa kwenye ofisi za mawakala walioteuliwa na Meneja wa Mfuko katika masaa ya huduma za kibenki katika siku za kazi (kuanzia saa 3 asubuhi mpaka saa 10 alasiri);

g) Maombi ya mauzo ya vipande yatakayo pokelewa na kukubalika katika ofisi za mawakala wakati wa masaa ya kazi, yataongozwa na thamani halisi ya vipande kwa siku ya kazi itakayofuata ;

h) Mkataba wa mauzo ya vipande utahesabika kuwa umekamilika siku ambapo maombi yamepokelewa isipokuwa tu kama maombi yatakataliwa na Meneja;

i) Kwa mauzo ya vipande baada ya mauzo ya mwanzo, mwekezaji atapata taarifa ya akaunti yake (SOA) ambayo itatumwa kwake si zaidi ya siku kumi za kazi kutoka siku ya kupokelewa maombi.

25.2 UWEKEZAJI WA NYONGEZA (ADDITIONAL INVESTMENT)

Uwekezaji wa nyongeza unaruhusiwa katika akaunti ya mwekezaji kama ifuatavyo:

- Kiasi cha Sh. 15,000/- kwa mwekezaji aliye katika mpango wa gawio (mapato)
- Kiasi cha Sh. 5,000/- kwa mwekezaji wa mwaka wa kukua hakuna kima cha juu cha uwekezaji.

25.3 MANUNUZI YA VIPANDE (REPURCHASE OF UNITS)

Mwekezaji ataweza kuiuzia UTT vipande vyote au baadhi ya vipande kuanzia tarehe 16 Aprili, 2009. Kuanzia tarehe hiyo, Meneja (Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT)) anaweza kununua vipande kutoka kwa mwenye vipande kwa thamani halisi ya kipande baada ya gharama za mauzo kuzingatia taratibu za kipindi cha kufungwa mfuko kama ilivyoelezwa kwenye ibara/kipengele 12 kwenye Waraka huu.

Mchakato wa manunuzi ya vipande utakuwa kama ifuatavyo:

- a) Manunuzi ya vipande yatafanywa kwa bei ya kununulia ambayo itafikiwa baada ya kupunguza gharama za kujitoa kwenye mfuko kutoka kwenye thamani halisi ya kipande kwa wakati huo;
- b) Mwekezaji anashauriwa/anatakiwa kuzingatia thamani halisi ya kipande wakati anatafakari kuuza vipande vya Mfuko wa Kujikimu wakati auzapo vipande vyake kwa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT). Iwapo atakuwa na mashaka anashauriwa kupata ushauri kutoka kwa wataalam wa maswala ya fedha;
- c) Iwapo mwekezaji anaamua kuuza vipande, atapaswa aende kwenye ofisi ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) au kwa mawakala walioteuliwa na Meneja wa Mfuko na atapewa fomu ya maombi na taarifa nyinginezo;
- d) Mwekezaji atapaswa kujaza fomu ya maombi ya kuuza vipande vya Mfuko wa Kujikimu;
- e) Fomu ya maombi ipelekwe kwenye ofisi za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) au kwa wakala yeyote aliyeteuliwa na Meneja

wa Mfuko ikiambatanishwa na taarifa ya Akaunti:

- f) Maombi ya mauzo ya vipande yatachukuliwa kuwa yamepokelewa siku husika ikiwa tu yatakuwa yamepokelewa na kukubaliwa kwenye ofisi za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) au mawakala walioteuliwa na Meneja wa Mfuko katika masaa ya huduma za kibenki katika siku za kazi (kuanzia saa 3 asubuhi mpaka saa 10 alasiri);
- g) Maombi ya mauzo ya vipande yatakayopokelewa na kukubalika katika ofisi za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) au mawakala wakati wa masaa ya kazi, yataongozwa na thamani halisi ya vipande kwa siku ya kazi itakayofuata;
- h) Kama uuzaji wa vipande vya mwekezaji utasababisha kufanya vipande kuwa vidogo chini ya kiwango cha chini kama ilivyoelezwa kwenye Waraka wa Toleo katika mpango wowote ule, basi vipande vilivyobaki vitawekezwa katika mpango wa ukuaji wa mwaka.
- i) Dhamana ya Uwekezaji Tanzania itatuma fedha za mauzo ya vipande kwa waliouza sehemu ya vipande katika kipindi kisichozidi siku kumi za kazi baada ya siku ya kupokea maombi kama ifuatavyo:
 - Wenye vipande ambao taarifa zao za benki zinajulikana watalipwa kwa kutumiwa fedha kwenye akaunti zao za benki.
 - Walipwaji ambao hawajatoa taarifa zao za benki watalipwa kwa njia ya posta (hawala ya fedha).

Muhimu: (i) Ikumbukwe kwamba ni lazima kwa wamiliki wa vipande watakaofanya mauzo ya baadhi ya

vipande zaidi ya Sh. 100,000/- kutoa taarifa zao za benki ambapo malipo ya mauzo yao yatatumwa kwenye akaunti zao za Benki.

- j) Pale ambapo fedha zitarudishwa baada ya kutumwa kwa njia ya benki au posta mwenye vipande hatadai fidia yoyote kutokana na kuchelewa kwa malipo yake.

26. DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA HAIRUHUSIWI KUWEKEZA KATIKA "MFUKO WA KUJIKIMU".

27 MAONI / MALALAMIKO YA WAWKEZAJI

Kama kuna maoni au malalamiko yoyote juu ya uendeshaji wa mfuko huu, tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:-

DHAMANA YA UWEKEZAJI TANZANIA

Jengo la Sukari, ghorofa ya pili,
Makutano ya Mtaa wa Sokoine na Ohio,
S.L.P 14825,
DAR ES SALAAM

Simu: +255 22 2128460/2128461

Simu za Bure:

(Tigo kwa Tigo) 0715 800 455 au 0715 800 544

(Voda kwa Voda) 0754 800 455 au 0754 800 544

Faksi: +255 22 2137593

Barua pepe: uwekezaji@utt-tz.org

Tovuti: www.utt-tz.org

Muhimu: Fomu maalum ya malalamiko ya mwekezaji inapatikana katika ofisi za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania au wakala walioteuliwa na pia katika tovuti ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania.

Itakapotokea mwekezaji hatoridhishwa na majibu ya Meneja basi anaweza kufikisha malalamiko yake katika Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa maamuzi. Endapo mwekezaji au meneja hataridhika na

majibu/maamuzi ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, basi watakuwa huru kwenda mahakamani.

28. GHARAMA ZA MFUKO

Gharama zifuatazo zitalipwa kutokana na mapato ya mfuko:

- Kodi kulingana na viwango vya kodi vinavyotumika.
- Ada zote kama itakavyoelekezwa na taasisi husika kama vile Soko la hisa.
- Ada ya ushauri wa uwekezaji ya asilimia moja na nusu (1.50%) ya Thamani ya Mfuko.
- Ada ya Mwangelizi wa mfuko ambayo itatozwa kwa mwaka kama ifuatavyo:

	Thamani ya Mfuko [Assets Under Management]	Gharama kwa mwaka
i	Kuanzia Sh 1.00 hadi Sh. bilioni 20	(d) 0.1 % ya Thamani ya Mfuko ilimradi ukomo usiwe chini ya Sh. milioni 20
ii	Kati ya Sh. bilioni 20 hadi Sh. bilioni 40	(e) 0.1 % ya Thamani ya Mfuko ilimradi ukomo usiwe chini ya Sh. milioni 30
iii	Zaidi ya Sh. bilioni 40	(f) 0.1 % ya Thamani ya Mfuko ilimradi ukomo usiwe chini ya Sh. milioni 50

- Gharama zingine ni asilimia sifuri nukta tisa (0.9%) ya thamani ya mfuko. Hizi ni gharama za kawaida katika uendeshaji wa shughuli za kila siku kama vile:

- Gharama za kuuza pamoja na matangazo.
- Gharama za benki
- Gharama ya ukaguzi wa hesabu
- Gharama za mwanasheria

- e) Gharama zinazohusiana na uuzaji na ununuzi wa vipande
- f) Gharama zinazohusiana na huduma kwa wenye vipande.

Hata hivyo, gharama zinginezo zinazohusiana na uendeshaji wa mfuko kama zilivoonyeshwa hapo juu zitakuwa na ukomo wa 2.4% ya Thamani ya Mfuko. Katika hali ambayo gharama zitazidi 0.9% ya Thamani ya Mfuko, basi kiasi kitachozidi kitalipwa na Meneja wa Mfuko.

Vile vile ikumbukwe kwamba gharama zote za mauzo ya awali na za mwaka wa kwanza zitagharimiwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) na kwa mauzo ya baadaye zitagharimiwa na Mfuko wenyewe.

Makisio ya gharama za mauzo ya awali zimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo hapa chini:

	MATUMIZI	MAKISIO YA GHARAMA (SH. MILIONI)
1.	Elimu kwa umma na mafunzo	80.00
2.	Matangazo	150.00
3.	Maandalizi na gharama za uchapishaji	31.50
4.	Gharama za kuandaa daftari la wenye vipande	75.00
5.	Mwanasheria/ Mkaguzi wa mahesabu	5.00
6.	Gharama nyinginezo	15
	<<<<<JUMLA>>>>>	Milioni 356.50
Muhimu: Zaidi ya gharama hizo hapo juu, pia kuna gharama za kamisheni za uwakala wa kukusanya mauzo ambazo ni kati ya asilimia 2 mpaka 2.25 ya mauzo.		

29. GHARAMA KWA WAWKEKEZAJI

29.1 GHARAMA ZA KUJITOJA

Meneja atatoza gharama za kujitoa kwenye mfuko kwa kupunguza kutoka kwenye thamani halisi ya kipande wakati huo ili kupata bei ya kununulia kipande kama ilivyoonyeshwa hapo chini. Gharama ya kujitoa itakuwa na kima cha chini cha Sh.500 kwa kila uuzaji.

- a) Zaidi ya mwaka mmoja tangu tarehe ya kuwekeza : 2% ya thamani halisi ya kipande.
- b) Zaidi ya mwaka wa kwanza na chini ya mwaka wa pili tangu tarehe ya kuwekeza: 1.5% ya thamani halisi ya kipande
- c) Zaidi ya mwaka wa pili na chini ya mwaka wa tatu tangu tarehe ya kuwekeza: 1% ya thamani halisi ya kipande
- d) Baada ya miaka mitatu tangu tarehe ya kuwekeza: Hakuna gharama za kutoka.

30. JINSI YA KUTATHMINI THAMANI HALISI YA MFUKO

THAMANI HALISI YA MFUKO (NET ASSET VALUE)

Thamani halisi ya mfuko, itapatikana kwa kuthaminisha rasilimali zote za mfuko na kutoa madeni yote baada ya kuzingatia mapato ambayo yanajulikana lakini hayajapokelewa na gharama zinazokisiwa. Thamani halisi ya kipande itatafutwa kwa kugawanya thamani halisi ya rasilimali zote za mfuko kwa idadi ya vipande kwa wakati huo.

Thamani halisi ya kipande itatangazwa katika tarakimu nne za desimali. Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itatangaza Thamani halisi ya mfuko katika siku zisizozidi 60 tangu kufungwa kwa mauzo ya awali.

Wakati wa kipindi cha utulivu (cool off period) thamani ya kipande itatolewa kila wiki na baadaye kila siku ya kazi kwa mauzo yajayo.

- a) Thamani halisi ya kipande itatolewa katika vyombo vya habari kwa kutangazwa, kila ijumaa ya kila juma kwa kipindi cha utulivu

na baada ya hapo katika kila siku ya kazi.

- b) Thamani halisi ya kipande itatangazwa katika magazeti yanayosomwa kwa wingi nchini.
- c) Thamani halisi ya kipande itakuwepo pia katika tovuti ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (www.utt-tz.org).
- d) Iwapo, katika siku yoyote ya kuthamani thamani ya mfuko, Soko la Hisa la Dar es Salaam litakuwa limefungwa kwa sababu ya sikukuu au sababu nyingine yoyote, bei za siku iliyotangulia zitachukuliwa kama ndio thamani halisi ya kipande/mfuko.

31. HAKI ZA WAMILIKI WA VIPANDE

- a) Haki ya kufaidika na rasilimali za Mfuko na mtawanyo wa vipande kulingana na walichowekeza katika Mfuko
- b) Wenye vipande wanayo haki ya kuiomba Dhamana ya Uwekezaji Tanzania habari yoyote ambayo inaweza kuwa na matokeo mabaya juu ya rasilimali zao, na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania itawajibika kutoa habari hiyo kwa wamiliki hao.
- c) Muhtasari wa Taarifa ya Mwaka kuhusu maendeleo ya Mfuko, utatumwa kwa wenye vipande, siyo zaidi ya miezi minne tangu tarehe ya kufungwa kwa mwaka wa fedha husika, na utakuwa tayari kwa kukaguliwa katika ofisi za Dhamana ya Uwekezaji Tanzania na matawi ya CRDB Bank Plc.
- d) Taarifa za mwaka wa fedha wa mfuko utaishia tarehe 30 Juni kila mwaka.
- e) Mabadiliko yoyote katika vipengele muhimu vya Mfuko yatafanywa pale tu wenye vipande watakapoamua kutoka kwenye Mfuko kuruhusiwa kuuza vipande

vyao kwa bei ya thamani halisi ya kipande kwa wakati huo. Wenye vipande watajulishwa kupitia matangazo kwenye magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchini kote.

- f) Wenye vipande wanayo haki ya kukagua nyaraka zifuatazo katika ofisi ya Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT):
 - (i) Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1994 (kama ilivyorekebisha).
 - (ii) Taratibu/kanuni za mipango ya uwekezaji wa pamoja za Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ya mwaka 1997.
 - (iii) Waraka wa makubaliano wa Mfuko wa Kujikimu.
 - (iv) Sheria ya Dhamana namba 318.

32. KODI

Maelezo yafuatayo ni kwa taarifa za jumla kwa wawekezaji. Taarifa sahihi kuhusu mambo ya kisheria na kodi, kila mwekezaji anashauriwa kupata ushauri wa mwanasheria au mshauri wa kodi.

Kulingana na sheria ya kodi inayotumika wakati wa kutoa waraka wa toleo hili, kodi zitakazotozwa zitakuwa kama:

- Mapato ya mfuko yatokanayo na riba yatatozwa kodi ya zuio ya asilimia 10 % ambayo itakakuwa ni kodi ya mwisho.
- Mapato yatokanayo na gawio kutoka kwenye hisa zilizooodheshwa yatatozwa kodi ya asilimia 5% badala ya asilimia 10%.
- Ongezeko la thamani kwenye hisa zilizooodheshwa kwenye Soko la Hisa Dar Es Salaam na hati fungani za serikali zenye kumilikiwa na Mfuko hazitatozwa kodi.

33. UKOMO KWA MFUKO.

Mfuko unaweza kufikia ukomo:

- (i) Iwapo itaamuliwa hivyo kwenye mkutano mkuu usiokuwa wa kawaida.
- (ii) Iwapo itakuwa kwa mujibu wa kifungu namba 122 na 124 cha sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

34. MAMBO YA JUMLA

- a) Maombi ya kununua vipande katika mazingira yafuatayo, yanaweza kukataliwa na Meneja endapo:
 - (i) Maombi yamepokelewa pamoja na fedha pungufu ya kima cha chini kinachoruhusiwa kwa ajili ya kununua vipande.
 - (ii) Fomu ya maombi haikutiwa saina na mwombaji.
 - (iii) Hundi iliyopelekwa benki ikiwa ni pamoja na maombi imekataliwa na malipo hayakupokelewa na Meneja.

- b) Uamuzi wowote wa Dhamana ya Uwekezaji Tanzania kuhusu kustahili au kutostahili kwa mwombaji kujiunga na Mfuko, utakuwa ni wa mwisho baada ya kuthibitishwa na Mamlaka. Kurejeshwa kwa fedha ya maombi yaliyokataliwa kutafanyika baada ya taratibu za kiutendaji kutekelezwa kwa gharama ya mwombaji na Meneja hatawajibika kulipa riba au kiasi kingine chochote cha fedha.

- c) Wamiliki ambao umiliki wao umetokana na udanganyifu katika maelezo yao, utafutwa na majina yao kuondolewa katika daftari la wenye vipande. Katika hali kama hiyo, Meneja atakuwa na haki ya kununua tena umiliki wa vipande hivyo kwa bei ya mwanzo au katika thamani halisi ya kipande ya wakati huo kutegemea bei ipi itakuwa ndogo kati ya hizo, baada ya kutoza kiasi ambacho ni sawa na asilimia kumi (10%) ya bei ya kununulia kama adhabu. Meneja anaweza kuchukuwa mgawanyo wa mapato, kama upo, ambao ulilipwa kwa wenye vipande wa namna hiyo kwa makosa na kulipa kiasi hicho kwa mwekezaji anayestahili.



KIAMBATANISHI – I

SEHEMU – I: MAELEKEZO YA JUMLA:

1. Tafadhali rejea taarifa zilizotolewa kwenye Waraka wa Toleo. Mwombaji awasiliane (kama atahitaji) na ofisi za mawakala waliosajiliwa wa Soko la Hisa la Dar es salaam, meneja wa benki, mhasibu, wataalamu na washauri wa masuala ya uwekezaji, au mwanasheria atakapojaza fomu ya maombi ya kujiunga.
2. Mfuko utakuwa wazi kwa mauzo ya mwanzo kuanzia 03 Novemba mpaka 29 Novemba, 2008
3. Jaza taarifa zote kwakutumia **HERUFI KUBWA**. Tumia kisanduku kimoja kwa kila herufi. Maombi yafanywe kwenye fomu halisi tu nakala, faksi au durufu zozote hazitapokelewa.
4. Wakati wa mauzo ya mwanzo vipande vitauzwa katika ofisi za mawakala zifuatazo;

Benki ya CRDB, Benki ya Exim, Benki ya Akiba, Benki ya Posta, Shirika la Posta na Mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam -Tanzania Securities, Solomon Stockbrokers, Rasilimali Ltd, Orbit Securities, Vertex International Securities Ltd & Core Securities Limited.
5. Kumbuka, usitoe pesa kwa mtu yeyote asiye wakala aliyeteuliwa, na baada ya kukabidhi pesa na fomu ya maombi hakikisha unapata risiti kutoka kwa wakala aliyepokea maombi yako na fedha.
6. Kila fomu ya maombi iambatanishwe na pesa taslimu au hundi itakayolipwa kwenye akaunti ya “Mfuko wa Jikimu”. Namba ya maombi iandikwe nyuma ya hundi

itakayotumika kufanya manunuzi ya vipande. (kama manunuzi yatafanywa kwa hundi).

7. Fomu ya mauzo ikishajazwa iwasilishwe pamoja na pesa kwa wakala wa kukusanya fedha waliotajwa hapo juu.
8. Mabadiliko yoyote katika fomu ya maombi yathibitishwe kwa sahihi kamili ya mwombaji.
9. Maombi yote yakishawakilishwa hayata rudishwa kama ilivyoainishwa kwenye waraka wa toleo.
10. Baada ya mauzo ya mwanzo wamiliki halali wa vipande watatumiwa Taarifa ya Akaunti kuonyesha idadi ya vipande wanavyomiliki.
11. Mauzo yanayofuata: Mfuko utakuwa wazi kwa mauzo ya vipande kuanzia tarehe 16 April, 2009 baada ya kipindi cha utulivu wa mfuko cha miezi mine na nusu tokea tarehe ya mauzo ya mwanzo.
12. Dhamana ya uwekezaji Tanzania ina haki ya kukataa maombi yoyote. Maamuzi yoyote ya Dhamana ya Uwekezaji juu ya stahili au kutostahili kumiliki vipande ni ya mwisho baada ya kupata uamuzi wa Waziri.
13. Kumbuka, ni muhimu kuweka sahihi kwenye fomu yako ya maombi kwani maombi yasiyo na sahihi hayatakubaliwa.

SEHEMU – II: TAARIFA ZA TOLEO:

MAMBO MUHIMU KUHUSU MFUKO WA KUJIKIMU:

- **Madhumuni:** Mfuko wa Kujikimu unalenga kutatua tatizo la kifedha kwa wawekezaji

ambao wanahitaji mapato ya mara kwa mara na wakati huo huo wakiangalia uwezekano wa kupata ukuaji wa mitaji yao kwa muda mrefu.

- **Aina za Uwekezaji:** Mfuko unatoa fursa tatu za uwekezaji - (a) Mapato ya kila robo mwaka (b) Mapato ya kila mwaka c) Ukuaji wa vipande (growth option)
- **Nani anaruhusiwa kuwekeza:** Mfuko uko wazi kwa watanzania walio ndani na nje ya nchi, watu binafsi, makampuni/taasisi, mabenki, asasi za kiraia, kama inavyoonyeshwa kwenye waraka wa toleo..
- **Thamani ya Mwanzo ya Kipande:** Thamani ya mwanzo ya kipande (face value) ni Sh.100/=.
- **Bei ya Kipande (Issue Price):** Vipande vitauzwa kwa bei ya Sh. 100/= kwa kila kipande wakati ya mauzo ya awali (kuanzia 3 Novemba 2008 mpaka 29 Novemba, 2008) na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani halisi.
- **Kima cha chini cha kuwekeza:** Ni Sh. milioni 2 kwa mpango wa mapato ya robo mwaka, na Sh. Milioni 1 kwa mpango wa gawio kwa mwaka na Sh. 5,000 kwa mpango wa kukuza mtaji.
- **Uwekezaji wa nyongeza:** Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza/unaofuata (additional investment) ni Sh.15,000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh. 5,000 kwa mpango wa ukuaji wa mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza
- **Ukwasi:** Ununuzi na Uuzaji wa vipande utafanyika kila siku ya kazi kuanzia tarehe 16 Aprili, 2009 yaani miezi mine na nusu baada ya kufungwa kwa kipindi cha mauzo ya awali. Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itatuma malipo ya mauzo ya vipande ndani ya siku 10 za kazi tangu kuwasilishwa kwa maombi ya mauzo
- **Uwazi:** Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itafanya tathmini na kutangaza thamani halisi ya kwanza ya mfuko (Net Asset Value) katika kipindi kisichozidi siku 60 tangu kufungwa kwa mauzo ya awali na baadaye itatathmini na kutangaza kila siku ya kazi. Hali kadhalika, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT) itatoa mgawanyo wa uwekezaji (Investment portfolio) kila robo mwaka.
- **Uhamishaji wa vipande :** Uhamishaji wa vipande kutoka kwenye mfuko mmoja kwenda mwingine kati ya mifuko inayoendeshwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania unaruhusiwa. Uhamishaji huu utatumia thamani halisi ya kipande kwa wakati huo bila gharama yoyote. Uhamishaji huo utafanywa kwa mauzo ya vipande kutoka kwenye mfuko mmoja na kuviwekeza kwa kununua vipande kwenye mfuko mwingine, ilimradi sifa za kuwekeza kwenye mfuko mwingine zimezingatiwa.
- **Makato ya Kodi:** Kulingana na sheria za sasa, kodi ya mapato haitotozwa kwenye gawio litokanalo na uwekezaji kwenye mfuko huu.
- **Kuorodheshwa:** Kwa sababu ni mfuko uliowazi ambapo manunuzi na mauzo ya vipande yatafanywa wakati wote na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (UTT), vipande vya mfuko havitapendekezwa kuorodheshwa kwenye soko lolote la hisa. Hata hivyo, hapo baadaye Meneja wa mfuko, baada ya kushauriana na Mwangalizi wa Mfuko na maombi yake kupitishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, ana uwezo wa kuamua kuorodhesha vipande vya mfuko kwenye masoko ya hisa.